



**JAMHURI YA MUUNGANO WA
TANZANIA
WIZARA YA MAJI**



**MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA
MAZINGIRA MUSOMA**

MKATABA WA AJIRA YA KAZI YA KUFUKUA MTARO WA BOMBA PAMOJA NA KUCHIMBA MTARO KWA AJILI YA KULAZA BOMBA KUU LITAKALOKHUKUA MAJI KUTOKA KATIKA BOMBA KUU LILILOLAZWA NA MKANDARASI, JANDU PLUMBERS LTD NA KUYAPELEKA KATIKA TANGI LILILOJENGWA KATIKA KILELE CHA MLIMA KWANGWA

KATI YA

BW. Paulo Chini Shamba

NA

MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MUSOMA

(MUWASA)

Mkataba huu umefanyika leo tarehe 06..... Mwezi 05..... Mwaka 2022.....

Kati ya

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Musoma (MUWASA) S.L.P 233 Musoma (ambaye katika mkataba huu anajulikana kama "Mwajiri")

Na

Bw. PAULO C. SHIMBA..... mwenye simu namba 0627073393... (Ambaye katika mkataba huu anajulikana kama "Mwajiriwa/Mchimbaji wa Mtaro")

1. AINA YA MKATABA

MKATABA WA AJIRA YA KAZI YA KUFUKUA MTARO WA BOMBA MAENEO YA MUSOMA CLUB MPAKA KATIKA STOO YA MUWASA ILIYOPO MWISENGE PAMOJA NA KUCHIMBA MTARO KWA AJILI YA KULAZA BOMBA KUU LITAKALOCHUKUA MAJI KUTOKA KATIKA BOMBA KUU LILILOLAZWA NA MKANDARASI, JANDU PLUMBERS LTD NA KUYAPELEKA KATIKA TANGI LILILOJENGWA KATIKA KILELE CHA MLIMA KWANGWA

KUANZA KWA MKATABA

Utekelezaji wa mkataba huu utanza mara baada ya mkataba huu kusainiwa.

2. ENEO LA KAZI

Kazi tajwa hapo juu itafanyika katika maeneo ya Kwangwa, Musoma Club mpaka Mwisenge.

3. MALIGHAFI ZA UTEKELEZAJI WA KAZI MAALUM

Mwajiriwa atatekeleza kazi tajwa hapo juu kwa kutumia vifaa vyake mwenyewe.

4. MAELEZO YA UTEKELEZAJI WA KAZI

Mwajiriwa atafanya kazi zifuatazo.

- a) Kuchimba mtaro kwa ajili ya kufukua bomba zenye kipenyo cha milimita 300
- b) Kusaidiana na mafundi wa MUWASA katika kung'oa bomba na kuziondoa kwenye mtaro aliofukua
- c) Kufukua mtaro aliofukua
- d) Kuchimba mtaro kutoka katika bomba kuu lililolazwa na Mkandarasi, Jandu Plumbers Ltd maeneo ya Kwangwa mpaka kwenye tangi lililojengwa katika Kilele cha Mlima Kwangwa

5. GHARAMA YA KAZI MAALUM

Gharama za kazi zote atakazofanya Mwajiriwa ni Shilingi za Tanzania **6,929,000.00** kama ilivyochanganuliwa katika jedwali hapo chini.

Jedwali: Mchanganuo wa Gharama za Kazi

Na.	Aina ya kazi	Sifa za Mtaro		Gharama Kwa kila Mita Moja ya Urefu wa Mtaro (TZS)	Jumla ya Urefu wa Mtaro (m)	Gharama kwa Wote (TZS)
		Upana (m)	Kina (m)			
1	Kufukua na kusadia mafundi wa MUWASA katika kukata na kuondoa bomba kwenye mtaro pamoja na Kufukia mtaro	0.6	1.0	7,000	347	2,429,000
2	Kuchimba mtaro kutoka katika bomba kuu lililolazwa mpaka kwenye tangi lililojengwa katika Kilele cha Mlima Kwangwa	0.6	1.0	5,000	900	4,500,000
Jumla Kuu						6,929,000/=

6. UTARATIBU WA MALIPO

- a) Mwajiriwa atalipwa malipo ya awamu kulingana na pendekezo la msimamizi wa mradi.
- b) Mwajiriwa atalipwa malipo yote kupitia benki. Ambapo mwajiriwa anatakiwa kupeleka akaunti namba katika ofisi ya uhasibu ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Musoma.

7. KUKOMA KWA MKATABA

Mkataba huu utafikia kikomo baada ya kazi kukamilika, kukaguliwa na kukabidhiwa kwa msimamizi wa mradi au kusitisha mkataba huu endapo mwajiri hataridhika na utendaji kazi/nidhamu ya mwajiriwa.

8. SHERIA ITAKAYOTUMIKA

Mkataba huu utaongozwa na kusimamiwa na sheria ya mikataba na sheria nyingine za Tanzania.

9. MAREKEBISHO YA MKATABA

Mwajiri na Mwajiriwa wanaweza kubadilisha baadhi ya masharti ya mkataba kwa makubaliano ya pamoja kwa njia ya maandishi.

